Ramani Ya Kanisa La Kristo

na

Ellis P. Forsman

Ramani Ya Kanisa La Kristo

na

Ellis P. Forsman

Machi 11, 2013

Ramani Ya Kanisa La Kristo

Math. 16:13-19

Watu wengi wanafahamu ramani. Wanatoa maelekezo, uwazi, n.k., inayoweza kufuatwa wakati wa kujenga. Inaweza kuwa vigumu kujenga nyumba bila ramani.

Wazo la ramani inarudi nyuma kwa Mungu

Mungu alimpa Nuhu maelekezo ya jinsi ya kujenga safina. Mwanzo 6:14-16, "*Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina ukaifunike ndani na nje kwa lami. Hivi ndivyo utakavyoifanya; mikono mia tatu urefu wa safina, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake. Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, ya tatu.*"

Kulikuwa na sababu ambayo Mungu alimtaka Nuhu kutengeza safina sawasawa na jinsi alivyoagiza. Kusudi la lami ilikuwa ni kuziba matundu ndani na nje ili kuzuia maji kuingia ndani ya safina. Unafikiri ingekuwaje kama Nuhu angeamua kutokutumia lami kwa sababu ilikuwa "inanata sana"?

Mungu pia akamwambia Nuhu kutengeneza safina kutoka katika mti wa mvinje. Leo, tunaweza kuiita mti wa saiprasi. Matokeo yangekuwa mabaya kama Nuhu angechagua kutumia aina nyingine ya mti kama mkaratusi au msira. Mungu alikuwa na sababu maalumu ya kumwambia Nuhu kutumia mti wa Mvinje; haijalishi kama tunafahamu kusudi lake, au hapana.

Mungu pia akamwambia Nuhu kutengeneza safina katika vipimo vya urefu 3000, vipimo 50 upana, na vipimo 30 kwenda juu. Kipimo kina urefu gani? Sawa, hiyo inategemea na sehemu na wakati iliyokuwa inatumiwa. Pia, kulikuwa na utofauti wa jinsi kiwango kilivyo kuwa kikipimwa. Mara nyingi kiwango kilikuwa kinapimwa kutoka katika kiwiko hadi kwenye vidole vya mkono; hii ili chukuliwa kama vipimo vifupi vya kiwango. Vipimo virefu vya viwango kutoka katika kiwiko hadi katika vidole vya mkono ukiongeza na upana wa kiganja.

Labda, kama unavyofahamu, urefu wa mkono wa kila mtu unatofautiana; hasa katika desturi za watu. Hataivyo, pia, kutoka katika ukufunzi wa mambo ya kale, urefu ulikuwa kama ifuatavyo:

Mfumo wa Vipimo Vya Urefu	Inchi	Sentimita
Ufupi wa kawaida	18"	45.72
Ufupi wa Kiyunani	17.5"	44.45
Urefu wa Kiyunani	19.8"	50.29
Ufupi wa Kimisri	17.6"	44.70
Urefu wa Kimisri	20.6"	52.32
Urefu wa Kibabeli	19.8"	50.29

Urefu wa Kibabeli, 19.8", (50.29) ilikuwa ni vipimo vya zamani vilivyorekodiwa, kama wakati wa Wababeli ulikuwa ukifuatiwa na wakati baada ya gharika na vipimo vingine vya urefu havikutokea hadi baadaye katika historia; ili kwamba vipimo viweze kuwa sahihi kabisa katika kuelezea vipimo vya safina. Ezek. 43:13 inaelezea urefu wa vipimo vya Kibabeli: "*Na vipimo vya madhabahu kwa dhiraa ni hivi; (dhiraa ni dhiraa na shubiri); tako lake ni dhiraa moja, na upana wake dhiraa moja ; na pambizo yake karibu na ncha yake pande zote, shubiri moja na hili litakuwa tako la madhabahu.*" Hiyo ingeweza kuifanya safina kuwa kati ya miguu 495 urefu, upana miguu 821/2, na kwenda juu miguu 49 ½ au kati ya 151 urefu, mita 25 upana, na mita 15 urefu kwenda juu.

Watengeneza mashuwa kwa miongo mingi wamegundua vipimo vya viwango vya safina ilikuwa kamili kuweza kusaidia mitumbwi mikubwa kuweza kuelea kwenye maji ya bahari, hata katika kimbunga. Kama walitaka kutengeneza safina mara mbili kama urefu, wangeweza kuunganisha upana na urefu wa mtumbwi. Kipimo kingine ambacho kingetumiwa kingearibu mtumbwi. Vipi kama Nuhu angeamua kutengeneza safina nusu ya upana? Hiyo ingeweza kusababisha matatizo mawili:

- Wanyama wote ambao Mungu alitaka wawe kwenye safina wasingetosha. Mungu alifahamu jinsi alivyotoa ramani ya safina ingekuwa kubwa kiasi gani.
- Pia, safina isingekuwa na uimara pembezoni. Kama safina ingegeuka kutokana na upepo ingeweza kuanguka kwa sababu ya

urefu wake. Mungu alijua alichokuwa anafanya alipotoa ramani ya safina.

Ndivyo ilivyo hata katika "Kanisa la Bwana". Tujifunze kilichojumuishwa katika ramani ya Kristo kwa ajili ya Kanisa lake.

Mungu ndiye mchoraji

Mwanadamu hawezi kuthibitisha chochote juu ya kile ambacho Mungu ametengeneza. Unafahamu kwamba Mungu aliweka kwa siri mpango wake wa Ufalme tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu? "*Ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema nitafumbua kinywa changu kwa mifano, nitayatamka yaliyositirika tangu awali.* (Mt. 13:35).

Kanisa halikuwa kitu ambacho alikufikiriwa; ili kuwa ni muhimu kwa Mungu. Kama mtu angebadilisha mpango wake, wangeangamizwa. "*Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze, mpate kuzishika amri za BWANA, Mungu wenu, niwaamuruzo.* (Kumb. 4:2). Pia, "*Usiongeze neno katika maneno yake; asije akakulaumu ukaonekana u mwongo.* (Mit. 30:6). Lazima wote tumfikie siku ya hukumu. Je unataka akuite mwongo siku hiyo kama "ukigeuza" mpango alioweka kwa ajili ya kanisa?

Mjenzi mmoja wa kweli ni Yesu Kristo

Yesu alisema atalijenga kanisa **Lake** , "*Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria – Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, watu hunena mwana wa Adamu kuwa ni nani? Wakasema, wengine hunena kuwa u Yohana mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmoja wapo wa manabii. Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simony Petro akajibu akasema, wewe ndiye mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe Simoni Bar Yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiye Petro na juu ya mwamba huu **nitalijenga kanisa langu**; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.* (Mt. 16:13-19).

Ni yesu Kristo pekee aliye na mamlaka ya kuweka msingi. Wengine wanadhani ni maendeleo mazuri kuzidisha au kupunguza katika mpango wake. Zingatia onyo ambalo Mungu alitoa katika Zaburi 127:1, "*BWANA asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure. BWANA asipoulinda mji, yeye aulindaye akesha bure.*" Kama tukijenga kitu ambacho Mungu hakutupatia, juhudi zetu hazifanyi cho chote. Sio tu

kwamba hazina cho chote, bali nafsi zetu zitapotea motoni. "*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.* (Ufu. 22:18-19).

Lazima tumkatae mjenzi mwingine ye yote isipokuwa Yesu Kristo

Wengine wanasema tunatoa muundo kwa kuwa thabiti. Wamekosea. "*Ingieni kwa kupitia mlango uliomwembamba maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingia kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani nao waionao ni wachache. Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya mwana kondoo walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.*" (Mt. 7:13-20).

Neno la Kiyunani inayomaanisha "imesonga" ni "*Stenos*" inayomaanisha "pakupitia pembamba".

Tamko la Kiyunani inayomaanisha "njia nyembamba" ni "*thlibo hodos*" ikimanisha "njia iliyozuiwa".

Hivyo, mtazamo wa kwanza ya jinsi tunavyopaswa kuwa makini ni kwamba lazima tufuate maagizo ya Mungu ya jinsi gani ya kufanyika Mkristo. Mtazamo wa pili jinsi gani tunapaswa kuwa makini katika maagizo yake ni kuishi maisha yetu ya kila siku na kumwabudu baada ya kufanyika Wakristo

Wengi wanapenda kufanya mabadiliko katika mpango wa Mungu wa Kanisa ili kwamba wengine wengi waweze kuwa wanakanisa. Hivyo, viongozi wa uongo wa kanisa wanapanua masharti ili kufanya kuingia huko iwezekane. Hii haikuwa mpango wa Mungu. Alitoa njia nyembamba kwa kusudi Lake.

Miaka ya nyuma iliyopita nilitaka kuwa na karakana ambayo ingeundwa jinsi nilivyotaka, hivyo nikachora ramani yangu na muundo na nikayatoa kwa uongozi wa mji ili kuweza kuzithibitisha. Nilitaka dirisha liwe upande wa kusini mwa karakana iliyotazama na barabara ili kwamba niweze kumwona mgeni yeyote akija kwangu. Magharibi mwa

karakana nikaweka sehemu ya kutunzia vifaa vya kazi, hivyo sikuweka madirisha upande huo. Kama mtu angelijenga karakana yangu, ningetaka waijenge sawasawa na jinsi nilivyotaka. Vipi kama mjenzi akifikiria mwenyewe kwamba "Magharibi mwa karakana kuna upenyo mkubwa, nadhani mwenye karakana atakuwa na furaha akiona mtazamo mkuu wa malisho ya farasi kutoka katika karakana yake." Nakubali kuwa hiyo ingekuwa mtazamo mkuu. Je ningekuwa na furaha? Hapana, nisingekuwa na furaha, kwa sababu ingeninyima nafasi ya stoo katika karakana yangu. Niliiunda kwa makusudi yangu, sio kwa sababu ya kile mtu anafikiria inaweza kuwa.

Tunapaswa kuzingatia kwamba Mungu anapotupatia maagizo ya jinsi ambavyo tunapaswa kuunda kitu, mawazo yake ni bora sana kuliko ya kwetu. "*Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki na aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa. Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.*" (Isa. 55:7-9)

Majengo mengine yote yataanguka!

Tunaambiwa na Yesu kwamba siyo watu "wema" wote wataokolewa. "*Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu. Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikapiga nyumba ile, isianguke kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.*" (Mt. 7:21-27).

Kwa nini Yesu aseme kwa ye yote anayedai kuwa amefanya ishara nyingi za ajabu kwa jina lake, "*Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu"*? Jibu lipo katika kitu hiki hiki ya ramani ya Mungu ambayo watu wengi wa dini wanaikataa – ubatizo. Ni pale tunapobatizwa ndipo dhambi zetu huoshwa, kwamba tunazidishwa katika kanisa, na majina yetu yanaandikwa katika kitabu cha Mwana Kondoo wa Uzima (Ufu. 3:5; 13:8; 17:8; na Fil. 4:3; Mk. 16:15-16; Mdo.

2:38-41; 8:12; 10:48; 22:16; Rum. 6:3-4; 1 Kor. 12:13; Gal. 3:27; 1 Pet. 3:21). Haijalishi kile tunachodai kufanya kwa jina lake; kama hatujabatizwa majina yetu hayaandikwi katika Kitabu cha Uzima; na kama haijaandikwa katika Kitabu cha Uzima; Atasema, "*Ondokeni kwangu siwajui ninyi mtendao mabaya".*

Anguko litakuwa kubwa ya wale wanaojenga kanisa juu ya mchanga.

Hakuna jengo ambalo ni imara kuliko msingi wake

Kanisa la Yesu Kristo lina msingi imara. Lilijengwa juu ya mwamba: Yesu Kristo. "*Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.*" (Mt. 16:16-17). Hatuwezi kuweka msingi mwingine, isipokuwa ule ambao tayari umeshawekwa. "*Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa mimi kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa yaani Yesu Kristo.*" (1 Kor. 3:10-11).

Damu iliyonunua kanisa lazima iwe katika msingi wa kweli. "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinua kwa damu yake mwenyewe.*" (Mdo. 20:28).

Muundo wa kanisa

Kanisa la Kristo halijajengwa kwa matofari, mawe, au mbao. Ni kundi la watu ambao ni wafuasi wake wa kweli. "*…Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*" (Mdo. 2:47). Pia, "*Ninyi nanyi kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho Mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.*" (1 Pet. 2:5). Kanisa ni mwili wa Yesu wa kiroho katika dunia ambayo anamamlaka kamili. "*Naye ndiye kichwa cha mwili yaani cha kanisa; naye ni mwanzo ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*" (Kol. 1:18). Kama ni mtangulizi katika mambo yote katika kanisa, je hiyo inatuachia cho chote ili tuwe watangulizi? Kanisa ni mwili wake kufanya kama inavyompendeza. "*Sasa nayafurahia mateso niliyonayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake.*" (Kol. 1: 24).

Yesu ndiye kichwa cha mwili, kanisa

Mungu alimpa Yesu mamlaka yote juu ya kanisa. "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*" (Efe. 1:22-23). Katika miili yetu ya nyama tunaviungo vingi; je tunaruhusu mikono yetu kuamua wanachotaka kufanya; au miguu yetu kuamua wanapotaka kwenda? Hapana, uamuzi huo hutoka katika vichwa vyetu; mikono yetu na miguu havina uwezo wa kufanya maamuzi. Hilo ni sawa na kanisa; sisi, kama mwili wake tunauwezo wa kufanya maamuzi; ambayo yote ni ya Kristo.

Kanisa linapaswa kuvaa jina la Kristo

Kanisa ni bibi harusi wa Kristo. "*Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendae mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye alivyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa.*" (Efe. 5:22-32).

Inaonekana kwako kwamba katika ndoa kati ya mwanamume na mwanamke kwamba asichukue (mwanamke) jina la mtu mwingine? Wanaume – mtajisikiaje kama ukioa mke wako akakuambia kwamba hataki kutumia jina lako, lakini badala yake akatumia jina la mtu mwingine mtaani? Mwanamume ye yote anaweza kuchukia kama mkewe anaitwa kwa jina la mtu mwingine. Je! Ulifahamu kwamba swala la mwanamke kuchukua jina la mwanamume linarudi nyuma kwa Adamu na Hawa? "*Mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina* ***lao*** *Adamu, siku ile walipoumbwa.*" (Mwa. 5:2). Binafsi, Mungu aliwaita Adamu na Hawa, lakini kama wanandoa, Mungu aliwaita Adamu.

Ni jina gani ambalo Biblia inaliita kanisa?

"*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*" (Mdo. 20:28). Tunaona kwamba kanisa liliitwa "*Kanisa la Mungu*". Ni damu ya nani iliyolinunua kanisa? Mungu Baba, au Mungu Mwana. Yesu alimwambia Petro angelijenga kanisa lake (Mat. 16:13-19).

Mtume Paulo katika barua yake kwa kanisa lililokuwa Rumi alitoa salamu nyingi katika sura ya 15; anahitimisha salamu katika mustari wa 16 kwa "*…Makanisa ya Kristo yawasalimu*." (Rum. 16:16). Alitambua kwamba kanisa ni la Kristo; nasi tunapaswa kufanya hivyo.

Je tunaruhusiwa kutumia majina mengine? Tunaambiwa tusitumie majina mengine. "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo, mtu huyu anasimama hali yu mzima mbele yenu. Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu kwa mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo*." (Mdo. 4:10-12). Yesu ndiye jiwe kuu la pembeni katika msingi wa Kanisa. Ni nini kusudi la jiwe la pembeni katika ujenzi leo? Lina tarehe ya utengenezaji, anayemiliki jengo, na mjenzi aliyeijenga.

"Hakuna jina lingine chini ya mbingu" ikimaanisha kwamba hakuna jina lingine ambalo halijatoka mbinguni. Tuna jina limeandikwa katika Agano Jipya ambalo lilitoka mbinguni. "Hakuna jina lingine…walilopewa wanadamu" inamaanisha majina ambayo mwanadamu uita kanisa. "Hakuna jina lingine…ambalo tunapaswa kuokolewa kwalo". Jina lina umuhimu gani? Mungu anasema linaumuhimu.

Hiyo inamanisha hatupaswi kutumia Lutherani, Pentekoste, Sabato, Katholiki, Kanisa lililokengeuka, au jina lingine lolote ambalo limeundwa na mwanadamu kwa ajili ya kanisa.

Efe. 2:19-22 inaiweka wazi jiwe kuu la pembeni ambayo Petro alikuwa anaizungumzia, ilikuwa ni jiwe kuu la pembeni, "*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaunganishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*"

Majengo yanayoinuliwa na jiwe la pembeni limekandamizwa katika mfumo wake; ina habari hizi zinazoelezea jiwe la pembeni: 1). Jina la mjenzi au mmiliki. 2). Mjenzi aliyejenga mfumo. 3). Tarehe ambayo jengo hilo lilijengwa.

Ni nani anayemiliki kanisa? **Yesu** (Mt. 16:18). Yesu ni kichwa cha nini? Cha Kanisa! (Efe. 1:22-23). Ni nani anayejenga kanisa? **Yesu** (Mt. 16:18. Kanisa lilijengwa lini? Siku ya Pentekoste, A.D. 30 (Mdo. 2). Ujumbe huu ndio unaoelezea jike la pembeni. Yesu ni jiwe la pembeni la kanisa. Hakuna jina lingine linaloruhusiwa chini ya mbingu, walilopewa wanadamu kwa ajili ya kanisa isipokuwa Yesu Kristo. Kanisa lilianzishwa mwaka wa 30 A.D. Na liliitwa Kanisa lake – Kanisa la Kristo kiujumla na makanisa ya Kristo kibinafsi. Hakuna jina lingine linaloruhusiwa kwa ajili ya kanisa. (Mdo. 4:10-12).

Jina langu ni Ellis Forsman; jina la mke wangu kabla hajaolewa aliitwa Lynell McCay; jina lake sasa ni Lynell Forsman. Kwa wakati huo alikuwa na nywele nyekundu; pia alitembea akichechemea, sasa kama ningepaswa kumwelezea kwa njia hiyo kwako, ungeweza kutambua kutokana na utambulisho huu kwamba ni mke wangu.

Jina la kaka yangu ni Evart Forsman; jina la mke wake ni Becky; ana nywele nyekundu na anatembea kawaida. Kama ungeweza kusikia kwamba jina lake la mwisho ni Forsman na kuona maelezo yake, ungeweza kusema kwamba huyo siyo mke wa Ellis Forsman.

Kuna makundi ya madhehebu leo ambayo yanavaa jina la Kristo, lakini maelezo yao hayaendani na bibi harusi wa Kristo katika Agano Jipya; hivyo basi, hawawezi kuwa bibi harusi wake.

Ramani ya kipekee inaonyesha jinsi mtu anavyofanyika Mkristo

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika kidato cha tano na sita (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu, akaniambia kwamba alikuwa haamini kwamba Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimesha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba kuna Mungu. Lakini ili awe sehemu salama labda aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mema Mungu

atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "haiendi hivyo. Unapaswa kumwamini kwa moyo wako wote bila hivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kutoka katika chumba kingine, unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani" taratibu unachukua simu ya mkononi, na kuwapigia polisi ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani mwako, unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo unawasikia wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwamba amekamatwa; sio kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angetubu kwamba hataiba tena na anataka kubadili maisha yake ili kwamba asije akaiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linalo leta badiliko la tendo. Hicho ndio tunafanya kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kukiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Zingatia katika kifungu hapo juu kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea katika kitu fulani; siyo kwamba tayari mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akakubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu ninayependezwa naye.*" Mt. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kufanya. Unaona jinsi ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema

"*Kwa kuwa itupasavyo kuitimiza haki yote*." Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, siyo kwa sbabu ni haki yetu. (Uamini katika haki + Ubatizo = Kuitimiza haki yote).

Tunayo maisha mapya katika ubatizo. Rum. 6:4, "*Basi* ***tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo*** *katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba,* ***vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.***" (Toba katika uzima + Ubatizo = Tunatembea katika upya wa uzima).

Ni katika ubatizo ndiposa tunafikia wokovu kwa kuoshwa dhambi zetu. Mk. 16:15-16, "*Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe.* ***Aaminiye na kubatizwa ataokoka*** *asiyeamini atahukumiwa.*" (Amini katika haki + kukiri katika wokovu + Ubatizo = Wokovu).

Yesu alimtuma Sauli kwa Anania na alimwambia cha kufanya ili aokolewe. Mdo. 22:16, "*Basi sasa, unakawilia nini? Simama,* ***ubatizwe, ukaoshe dhambi zako****, ukiliitia* ***jina lake***." (Kukiri katika wokovu + Ubatizo = Wokovu kutoka katika dhambi zako).

Hakika, tusipobatizwa, tusipobatizwa bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia, tubuni, kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2: 38). Petro, umesema ni nini kusudi la ubatizo? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu.

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu **lazima** tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Mk. 16:15-16).

Watu wananiambia kwamba Yesu alijali dhambi zao alipokufa msalabani na kwamba hawakuhitaji kubatizwa. Ndiyo, Yesu alikuwa na dhambi zangu msalabani alipokufa, lakini dhambi zetu bado tungali nazo isipokuwa sisi binafsi tukizizika.

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, huku ukiliitia jina la Bwana.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake,*

kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena;" (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu ya kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza". Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini, na kuuwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Ramani ya kipekee pia inaonyesha vitu ambavyo tunapaswa kufanya katika ibada

- **Imba.** Kila Agano Jipya inayohusisha muziki katika kanisa inasema "*imba*"; kama vile, "*Mkisemezana kwa saburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.*" (Efe. 5:19). Haisemi, "piga makofi", "piga ngoma", "piga kinanda", au chombo chochote kilichotengenezwa na mwanadamu. Ni kiburi tukifikiria tunaweza kufanya kitu kingine badala ya "*kuimba*". Tunaambiwa katika Zaburi 19:13, "*Umzuie mtumishi wako asitende mambo ya kiburi, yasinitawale mimi. Ndipo nitakapokuwa kamili, nami nitakuwa safi, sina kosa lililo kubwa.*" Wengine wanadai, "Ndiyo, lakini Daudi alipiga chombo cha muziki!" ndiyo, alipiga; lakini je Mungu alipendezewa? Hakika, hakupendezwa: "*Ole wao … Ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda vya namna nyingi, kama vile Daudi.*" (Amosi 6:1,5). Hatuwezi kumtumia Daudi kama mfano wa kutumia vyombo vya muziki…

- **Omba**. Wakati mtume Paulo alipokuwa akisafiri aliyaomba makanisa kuwaombea, "*Ndugu mtuombee."* (1 Thes. 5:25). Pia anasema waliyaweka makanisa katika akili zao katika maombi, "*Kwa hiyo twawaombea ninyi siku zote, ili Mungu wetu awahesabu kuwa mmekustahili kuitwa kwenu, akatimiza kila haja ya wema na kila kazi ya imani kwa nguvu; jina la Bwana wetu Yesu litukuzwe ndani yenu, nanyi ndani yake, kwa neema ya Mungu wetu na ya Bwana Yesu Kristo.*" (2 Thes. 1:11-12). Pia tunaombea kila mmoja. "*Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi. Mtu wa kwenu amekuwa hawezi?*

Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi atasamehewa. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii." (Yak. 5:13-16). Bunda Tanzania kulikuwa na vijana waliopotea. Walikwenda kwa siku chache; hakuna aliyefahamu walipokwenda. Swala hili lilienea katika baadhi ya makusanyiko Afrika ya Mashariki, na nikatuma taarifa kwa makusanyiko yaliyoko marekani. Maombi mengi yalimwendea Mungu kwa ajili ya usalama wa vijana hao wawili. Muda mfupi baada ya hilo, vijana hawa walitokea. Yale walioyasema yalitisha! Mtu mmoja aliwaambia, "kama mnataka, nina kazi inayoweza kuwalipa ninyi vijana; lakini tunapaswa kusafiri kwenda sehemu nyingine ili muweze kufanya kazi." Walikubali. Mtu huyu aliwapeleka kwa mganga wa kienyeji anayeua watu kwa ajili ya viungo vyao vya mwili. Wakati huo ndio maombi haya yote yalikuwa yakimwendea Mungu. Biashara kati ya mtu huyu na mganga wa kienyeji ikashindikana. Kawaida, biashara kama hii inaposhindikana, mtekaji nyara anaweza kuwaua mateka kwa sababu wanaweza kumtambua. Katika swala hili, mtekaji nyara aliwaruhusu vijana hawa kuondoka. Waliweza kufika nyumbani salama. Maombi yanafanya kazi!! Baba yao hakuwa Mkristo, lakini alivutiwa na jinsi maombi haya yote yalivyofanya kazi na akafanyika Mkristo muda mfupi baada ya vijana hawa kurudi nyumbani.

- **Tunapaswa kuomba na kuimba kwa roho na ufahamu.** "*Imekuwaje basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia.*" (1 Kor. 14:15). Tunapaswa kuimba na kuomba kutoka mioyoni mwetu na tunapaswa kufikiria kile tunachokiomba na kuimba. Nimewahi kusikia hili likitamkwa katika maombi ya baadhi ya washirika. "Bwana, tunakuomba ujibu maombi yote yaliyo katika mioyo ya matu". Tunawezaje kusema amina kwa kitu tusichokijua? Labda wengine wanaomba kwa ajili ya kitu ambacho wanataka kukimaliza kutokana na tama zao. Pia, nimewahi kusikia washirika wakiimba mistari katika nyimbo ambayo siyo ya kimaandiko. Tunapaswa kuwa makini na mambo haya.

- **Abudu siku ya kwanza ya juma.** Mdo. 2:1, "*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja.*" Siku ya Pentekoste mara nyingi ilitokea katika siku ya kwanza ya juma katika siku ya Wayahudi. Hiyo ni siku ambayo kanisa lilianza. Pia tunaambiwa

katika Mdo. 20:7, "*Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri sikua ya pili yake, naye akafululiza maneno yake hata usiku wa manane*." Tendo la ibada katika Agano La Kale siku ya Sabato ilikwisha wakati Yesu alipokufa msalabani.

Ellen White (mwanzilishi wa kanisa la wasabato) alidai kwamba malaika alimwambia siku ambayo tunapaswa kuabudu ni sabato, siyo Juma Pili: kwamba Wakatholiki wanakosea kwa kubadilisha siku ya kuabudu katika mwaka wa 325 A.D. katika Shauri la Nicea. Kuna matatizo kadhaa juu ya swala hili: (1) Neno "Katholiki" haijaonyeshwa katika mandiko yo yote kuhusu Shauri la Nicea. (2) Hakuna neno lilionyeshwa la "Papa" katika maandishi yo yote kuhusu Shauri la Nicea. (3) Kama Kanisa la KAtholiki lili kuwepo kwa wakati huo, papa ndiye angekuwa mtawala wa shauri hili, na siyo Konstantini, ambaye hakubatizwa hadi wakati alipokaribia kufa. (4) Kama kanisa la Katholiki lilikuwepo kwa wakati huo, mkutano huo ungefanyikia Rumi, siyo Nicea. Kanisa la Katholiki halikuwepo hadi mwaka 606 A.D. ilipoanzishwa na Boniface aliyetangaza kwamba alikuwa kiongozi wa mashemasi wote wa dunia.

Historia inathibitisha kwamba ushirika wa Wakristo katika ibada katika siku ya kwanza ya juma; vitu hivi vimeorodheshwa kubwa hadi ndogo kwanzia ya hivi karibuni (hadi shauri la Nicea katika 325 A.D.) kurudi nyuma wakati wa Mitume:

- Eusebius wa Kaisaria [319 A.D.] katika uthibitisho wa Injili 4:16: 186 aliandika "[S]iku yake [Kristo] mwanga …ilikuwa ni siku ya kufufuka kwake kutoka katika wafu, ambayo wanasema, ni moja na ya kipekee na hakika ni siku takatifu na siku ya Bwana, ni bora kuliko siku nyingine kama jinsi tunavyozielewa, zaidi ya siku zilizowekwa na sheria ya Musa kwa sherehe, mbalamwezi mpya, na sabato, ambayo Mtume [Paulo] anafundisha kwamba ni kivuli cha siku na siyo siku halisi".

- Eusebius wa Kaisaria [312 A.D.] katika historia ya Kanisa 1:4:8 aliandika "Wale[watakatifu wa kwanza wa Agano la Kale] hawakujali kuhusu kutahiriwa kwa mwili, hata sisi [Wakristo]. Hawakujali kuhusu kufuata Sabato, vile hata sisi. Hawakukataa kula aina fulani ya vyakulaa, au kuzingatia sheria ambayo Musa alitoa mwanzoni kuwa ishara; hata Wakristo wa siku hizi wanafanya mambo hayo".

- Victorinus [300 A.D.] Katika uumbaji wa Dunia aliandika, “Siku ya sita [Ijumaa] inaitwa mapito, hiyo ni kusema maandalizi ya ufalme… katika siku hii pia, katika hesabu ya siku ya mateso ya Bwana Yesu Kristo tunafanya taraja kwa Bwana au kufunga. Katika siku ya saba alipumzika katika kazi zake zote, akaibariki na kuitakasa. Katika siku za nyuma tuliambiwa tufunge kisawasawa, kwamba katika siku ya Bwana tunaweza kwenda katika mkate wetu kwa kutoa shukurani. Mtu na awe mfungaji sawasawa, tusije tukapatikana kuchunguza Sabato pamoja na Wayahudi…ambaye Sabato [Kristo] katika mwili wake aliutengua.

- Didascalia [225 A.D.], “Mitume walionyesha zaidi: Siku ya kwanza ya juma kuwepo na huduma, na kusoma maandiko matakatifu, na kuelewa, kwa sababu siku ya kwanza ya juma Bwana wetu alifufuka, na siku ya kwanza ya juma alifufuka juu ya ulimwengu, na siku ya kwanza ya juma alipaa mbinguni, na siku ya kwanza ya juma atakuja mara ya mwisho na malaika wa mbinguni”.

- Tertullian [204 A.D.]: “Kanisa la Kristo linalojumuisha waaminio waliobatizwa, hukutana kila siku ya kwanza ya juma kumega mkate wa Meza ya Bwana.”

- Tertullian [203 A.D.] ndani ya jawabu la Wayahudi 2 “[Y]eye ashindanaye kwamba Sabato bado inaangaliwa kama kigezo cha wokovu, na kutahiriwa siku ya nane …inatufundisha kwamba, kwa wakati uliopita, watu wenye haki waliitunza sabato au kutahiriwa, na hivyo wakatolewa kuwa “marafiki wa Mungu”. Kwa maana kama kutahiriwa kuna mwondoa mwanadamu, kwa vile Mungu alimfanya Adamu bila kutahiriwa, kwa nini Hakumtahiri, hata baada ya kutenda dhambi, kama kutahiriwa kunaondoa?... Hivyo basi, kwa vile Mungu alimtoa Adamu akiwa hajatahiriwa na hakuangalia Sabato, pia hata vizazi vyake navyo, Abili akiwa anatoa sadaka yake, hakutahiriwa na hakuchunguza Sabato, ilikuwa kwa ajili yake [Mungu] kusifu [Mwa.4:1-7, Ebr. 9:4]… Nuhu pia hakutahiriwa – ndiyo, pia hakuchunguza Sabato – Mungu alimwondoa katika dhoruba. Kwa Enoka pia, mtu mwenye haki sana, hakutahiriwa na hakuchunguza Sabato, alibadilika kutoka katika ulimwengu huu, ambaye mwanzoni hakuonja mauti ili kwamba akiwa mtahiniwa wa

uzima wa milele, atuonyeshe kwamba nasi twaweza, pasipo mzigo wa sheria ya Musa, tumpendeze Mungu".

- Justin Martyr, [155 A.D.] Katika msamaha wa kwanza, sura ya 67 aliandika: "…katika Siku inayoitwa juma pili, wote waishio katika miji au katika nchi hukusanyika pamoja na maandiko ya mitume au utabiri wa manabii usomwa, kwa kadiri muda unavyoruhusu…"
- Justin Martyr, [155 A.D.] pia aliandika katika tahariri pamoja na Trypho, 18, 21 "[S]isi pia tunapaswa kuangalia tohara ya mwili, na Sabato, na kwa ufupi sherehe zote, kama hatukujua ni kwa sababu gani hawakuungana na ninyi – jina katika hesabu ya makosa yenu na ugumu wa mioyo yenu…Inakuwaje, Trypho, kwamba tuyachunguze haki hizo ambazo hazitudhuru – ninaongelea tohara ya mwili na sabato na sikukuu?...Mungu hakuwaunganisha kuitunza sabato, na kuwapa ninyi mitazamo mingine ya ishara, kama nilivyo tangulia kusema, katika swala la kutokuwa na haki na ile ya baba zenu".
- Ignatius wa Antiokia [110 A.D.] katika barua kwa Magnesian wa 8 aliandika: "[W]ale waliolelewa katika mambo ya kale [kama vile Wayahudi] wamekuja katika tumaini jipya, hawashiriki sabato, bali wanaishi kwa kufuata siku ya Bwana ambapo pia uzima wetu ulirejeshwa na yeye na kwa kifo chake".
- Barnabas [74 A.D.] katika Barua ya Barnaba 15:6-8, "Tuantunza siku ya nane [Juma Pili] kwa furaha, siku ambayo pia Yesu alifufuka kutoka katika wafu".

Hata kama Ellem White alipokea ujumbe kutoka kwa malaika, Mtume Paulo katika Gal. 1:8-9 alisema kuikataa, "*Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyo wahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe*."

- **Meza ya Bwana.** Wakristo wa kwanza mara nyingi walishiriki meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma. "*Hata siku ya kwanza tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane.*" (Mdo 20:7). Pia, 1 Kor.

11:26-29, "*Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulae mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, ula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili.*"

- **Changizo.** "*Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake kwa kadiri ya kufanikiwa kwake, ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja.*" (1 Kor. 16:2). Tunaona kwamba matoleo yetu yafanyike siku ya kwanza ya juma; hakika, Kiyunani "Kata mien sabatoon" ikimaanisha "Kila siku ya kwanza ya juma".

- **Wanawake na wanyamaze katika kanisa.** "*Wanawake na wanyamaze katika kanisa maana hawana ruhusa kunena bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa.*" (1 Kor. 14:34-35). Usimlaumu mhubiri kwa kuonyesha kifungu hiki na pia usimlaumu Paulo kwa kuliandika, kwa sababu anasema ni agizo la Mungu. Lazima tukubali kila kitu ambacho Paulo aliandika kwa sababu alikuwa mtume aliyeongozwa na Roho Mtakatifu. "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo ilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.*" (1 Thes. 2:13).

Kanisa linauangalizi wa wazee

Efe. 4:11-12, "*Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;*"

Muinjilisti ni yule aliyesafiri na kuhubiri injili ya Kristo.

Wachungaji.

Katika Agano Jipya "*wachungaji*" inaonyeshwa tu katika kifungu hicho hapo juu. Neno la Kiyunani la "*wachungaji*" ni "poy- mane"; ikimanisha "kuangalia au kulisha kundi". "Poy-mane" pia hutafsiriwa kama "*waangalizi*" inapatikana mara 15 katika Agano Jipya.

"*Wachungaji*" na "*Waangalizi*" inaonyesha kitengo kile kile katika kanisa ambalo wanapaswa kulinda au kulisha kundi la Wakristo katika kusanyiko.

Katika Agano la Kale wachungaji na waangalizi pia ili kuwa na maana kama hii. Yer. 23:1-4, "*Ole wao **wachungaji**, wanaoharibu kondoo za malisho yangu na kuwatawanya! Asema BWANA. Kwa sababu hiyo BWANA Mungu wa Israeli, asema hivi, juu ya wachungaji wanaowalisha watu wangu. Mmetawanya kundi langu, na kuwafukuza, walahamkwenda kuwatazama; angalieni nitawapatiliza uovu wa matendo yenu, asema BWANA. Nami nitakusanya mabaki ya kundi langu, katika nchi zile zote zilizowafukuza, nami nitawaleta tena mazizini mwao; nao watazaa na kuongezeka. Nami nitaweka juu yao **wachungaji** watakaowalisha; wala hawataona hofu tena, wala kufadhaika, wala hatapotea hata mmoja wao, asema BWANA.*"

Neno la Kiebrania katika kifungu hiki la "*wachungaji*" ni "ra'ah"'; ikimanisha "kulinda au kutunza kundi". Neno la Kiebrania la "*waangalizi*" katika kifungu hiki pia ni "ra'ah"; "kuangalia au kulisha kundi".

Katika Agano la Kale na Agano jipya "wachungaji" na "waangalizi" inamanisha kitu kile kile – "kulisha au kutunza kundi." Ni wajibu ule ule.

Wazee.

"*Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa.*" (Mdo. 20:17). Katika mustari wa 28 Paulo aliwaagiza wazee wa kanisa, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*" Wazee walipaswa kulilisha kundi, kuliangalia, na kulichunga. Ni kazi ile ile ilyotolewa kwa wachungaji na waangalizi; vile vile, wachungaji, waangalizi, na wazee wako katika ofisi moja; (kazi zao ni moja).

Katika Tito 1:5-7 tunasifa kwa ajili ya ofisi ya wazee (wachungaji na waangalizi): "*Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopungua, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; Ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, anawatoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu;*" tunaona hapa kwamba wazee ni sawa na maaskofu; wale wanaoangalia kundi; askofu siyo mtu anayetoa maamuzi katika makusanyiko mengi. Askofu kirahisi inamanisha yule anaye angalia.

Hivyo askofu ni wale pia wanaoangalia na kulilisha kundi.

Yesu aliitwa mchungaji na askofu war oho zetu; zaidi sana akifunga majina hayo mawili katika ofisi moja: "*Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetukatika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. Kwa maana mlikuwa mnapotea kama kondoo; lakini sasa mmemurudia Mchungaji na Mwangalizi wa Roho zenu.*" (1 Pet. 2:24-25).

Hivyo tuna ofisi ile ile ya kulisha na kulitunza kundi ikiwa inaelezewa kwa majina manne tofauti: wachungaji, waangalizi, wazee, na maaskofu. Kila moja kati ya haya mara nyingi hutolewa kwa wingi; tendo la mwanamume mmoja kuitwa mchungaji akiongoza kusanyiko ni kinyume na maandiko.

Pia kuna mashemasi wa kanisa wanajali mahitaji ya kimwili ya kanisa. "*Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vyema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu.*" (1 Tim. 3:8-13).

Wote wazee na mashemasi lazima wajaribiwe kwanza kabla ya kuingia ofisini.

Tumeona hiataji la mashemasi katika kanisa katika Mdo 6:1-4, "*Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeaka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku. Wale Thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumia mezani. Basi, ndugu chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile neno.*"

Tunapata ofisi hizi zote zilijaa katika kanisa kule Filipi. "*Paulo na Timotheo watumwa wa Kristo Yesu, kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu, walioko Filipi, pamoja na maaskofu na mashemasi. Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.*" (Fil. 1:1-2).

Kuna ofisi mbili pekee katika kanisa: wale wanaoangalia au wanaochunga na kulilisha kundi (kusanyiko): wachungaji, waangalizi, wazee, au mashemasi; na wale wanaoangalia kwa kuhudumia mahitaji ya kimwili ya kusanyiko, maaskofu.

Tusifanye vitu vinavyotufanya kusimama nje kuliko kufanya kazi njema kwa ajili ya Bwana.

Mat. 23:5, "*Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu; kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao.*"

Mapadiri wa Kikatholiki na wengine upenda kufanya hili. Baadhi ya makundi ya dini huvaa suti nyeusi na kola shingoni kuwafanya wasimame nje. Wanafanya hili ili waonekane na watu wakidai, "Mimi ni mtu mwenye haki". Matendo yako mema yaonyeshe kwamba wewe ni Mkristo.

Mat. 23:27-28, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri bali ndani yamejaa mifupa ya wafu na uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi.*"

1 Tim. 2:9-10, "*Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi si kwa kusuka nywele wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za dhamani; bali kwa matendo mema kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu.*"

Hata wanawake wanaambiwa wasifanye vitu vya kuwafanya wasimame nje ya wengi kwa njia wanayovaa na kusuka nywele zao. Wanapaswa kuonyesha matendo mema kwamba wao ni Wakristo.

Usimuite mtu Baba, Kiongozi, au Mkuu

Mt. 23:9-10, "*Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo.*"

Waumini wa Sanhedrin wali sisitiza kuwa waitwe Baba au Wakuu kwa sababu ya "hekima na ujuzi waliokuwa nayo". Hii ndiyo matumizi ya Baba na Mkuu ambayo Yesu alimanisha tusiitwe.

Neno Takatifu imetumiwa tu mara moja katika Biblia: Zaburi 111:9 (mlango wa somo: Sifa kwa Mungu), "*... jina lake ni takatifu la kuogopwa.*" Ni Mungu pekee ndiye anaepaswa kuitwa Mtakatifu.

Hitimisho

Ninaamini kipeperushi hiki kimekupatia picha halisi ya ramani ya Mungu kwa ajili ya kanisa.